# Hakikisho la Kusoma la Gredi ya Tatu la Ohio ni nini?

Hakikisho la Kusoma la Gredi ya Tatu la Ohio ni sheria ambayo shule za Ohio lazima zifuate kuanzia Chekechea (Angalia Kanuni Iliyorekebishwa ya Ohio 3313.608).

Sheria hii inahitaji shule:

1) **Zipime stadi za kusoma** za watoto wote katika Chekechea hadi gredi ya tatu mwanzoni mwa kila mwaka wa shule.
2) **Ziambie familia kwa maandishi ikiwa mtoto wao hasomi kama inavyotarajiwa kwa kiwango chake cha gredi** kulingana na matokeo ya mtihani. Sheria inataja waziwazi maelezo ambayo shule zinapaswa kutoa kwa familia kuhusu matokeo ya mtihani na mpango wa shule wa kumfundisha mtoto kusoma shuleni.
3) **Zitoe maagizo maalum kwa mtoto, yanayoitwa huduma za kuingilia kati.** Huduma hizo zinapaswa kulenga mahitaji maalum ya kujifunza ya mtoto wako ikiwa alipata alama chini ya kiwango cha gredi kwenye mtihani. Huduma za kuingilia kati lazima ziwe na msingi wa **sayansi ya kusoma**.
4) **Unda Mpango wa Uboreshaji na Ufuatiliaji Kusoma ndani ya siku 60** za tarehe ambayo mtoto wako alipewa mtihani wa kusoma mwanzoni mwa mwaka. Mwalimu wa darasa la mtoto na mzazi/mlezi lazima washiriki katika uundaji wa mpango huu.

## Kwa nini tuna sheria hii Ohio?

Watoto ambao hawasomi katika kiwango cha gredi wana wakati mgumu shuleni wasipopata msaada wa ziada. Wana uwezekano mkubwa mara nne wa kuacha shule ya upili.

## Ninaweza kufanya nini ili kumsaidia mtoto wangu afike kiwango kinachotarajiwa?

Wazazi wanaweza kufanya mengi ili kumsaidia mtoto wao asome kila siku!

- **Sifu usomaji wa mtoto wako mara kwa mara.** Inafurahisha sana mtoto anapofanya maendeleo ya kusoma. Shiriki jinsi unavyojivunia ukuaji wake.
- **Mpe mtoto wako muda wa kufanya mazoezi ya stadi za kusoma na kuandika ambazo tayari amejifunza** shuleni. Waulize walimu wa mtoto wako stadi maalum unazohitaji kuboresha.
- **Msikilize mtoto wako wakati anaposoma.** Vitabu fulani, vinavyoitwa vitabu vya kusimbua, ni nzuri sana kwa kufanya mazoezi maalum ya kusoma. Muulize mwalimu au mkutubi mifano ya vitabu vinavyolingana na kile ambacho mtoto wako anahitaji kufanya mazoezi.
- **Akifanya makosa, mwambie asome neno hilo polepole tena.** Mwambie mtoto wako asome tena sentensi ili kuhakikisha kuwa anaelewa maana yake.
- **Ni sawa kupumzika kwa kutosoma ikiwa mtoto wako anahitaji hivyo. Jaribu kadi za ghibu, vifaa na michezo mingine ya kujifunza, au badala yake ujizoeze kuandika.** Kujifunza kunaweza kufanyika kwa njia nyingi tofauti.
- **Weka vitabu na vifaa vya kuandika katika maeneo yote ambayo mtoto wako hukaa kila siku.**
- **Ongea na mwalimu wa mtoto wako kila mwezi** au mara nyingi zaidi kuhusu jinsi kusoma kinavyoendelea nyumbani, na uulize kusoma kunaendeleaje shuleni.

Ohio Statewide Family Engagement Center at The Ohio State University

Ohio Department of Education & Workforce

## Maswali ya kumuuliza mwalimu

- **Shule imekusanya data gani** kuhusu kusoma na kuandika kwa mtoto wangu mwaka huu wa shule? Je, ninaweza kupata nakala ya matokeo? (Kumbusho kwa wazazi: Ikiwa matokeo yanakanganya, omba maelezo zaidi ili kukusaidia kuelewa.)
- **Nimtaala na nyenzo zipi zizonatumiwa na mtoto wangu** katika wakati wake wa kusoma na kuandika?
- **Nini hufanyika wakati wa kusoma na kuandika shuleni?** Je, mtoto wangu anaweza kuzingatia na kushiriki katika masomo? Je, anaonekana kufanya maendeleo? Ikiwa sivyo, shule inaweza kufanya nini kingine ili kumsaidia mtoto wangu ajifunze?
- **Mtoto wangu asipofanya maendeleo yoyote katika mwezi ujao**, nina chaguzi gani zingine ndani ya mfumo wa shule za kumtafutia mtoto wangu msaada zaidi?

## Je, mtoto wangu anaweza kwenda gredi ya nne asipopita Mtihani wa Kusoma?

Ndiyo. Shule zinaweza kupendekeza kwamba wanafunzi wengine warudie sehemu au mwaka wao wote wa gredi ya tatu kwa sababu ya kutofikia alama ya kiwango cha gredi ya kusoma katika darasa la tatu. Wanafunzi bado wanaweza kujiunga na gredi ya nne kulingana na misamaha ifuatayo katika sheria hii.

### Msamaha wa kutorudia gredi ya tatu

1) **Wazazi wanaweza kuomba mtoto wao ajiunge na gredi ya nne**, baada ya kuzungumza na mwalimu wa mtoto wao na mwalimu mkuu kuhusu alama zake za kusoma na chaguzi za kupokea usaidizi wa usomaji wake. Wazazi wana mamlaka ya mwisho ya uamuzi huu. Soma zaidi kuhusu msamaha huu kwenye tovuti ya Kituo cha Ushiriki wa Familia cha Ohio .
2) **Wanafunzi wanaopokea huduma za Lugha ya Kiingereza** wenye chini ya miaka mitatu ya msaada wa Lugha ya Kiingereza wanaweza kwenda darasa la nne.
3) **Wanafunzi wanaopokea huduma za Elimu Maalum** ambao IEP yao imeandikwa kwamba wamesamehewa.
4) **Wanafunzi wanaopokea huduma za Elimu Maalum** ambao tayari wamepata urekebishaji mkubwa katika kusoma kwa miaka miwili ya shule lakini bado hawasomi katika kiwango chao cha gredi.
5) **Wanafunzi ambao walipata urekebishaji mkubwa katika kusoma kwa miaka miwili ya shule na ambao tayari wamerudia kiwango cha gredi** katika Chekechea hadi Gredi ya Tatu.
6) **Wanafunzi wanaofikia alama za kupita kwenye mtihani mbadala** ulioidhinishwa na jimbo.

## Msaada gani hutolewa kwa wanafunzi baada ya gredi ya tatu?

Ingawa inaitwa hakikisho la kusoma la gredi ya tatu, shule lazima ziendelee kutoa msaada kwa wanafunzi ambao hawasomi katika kiwango cha gredi hadi gredi ya 12. Uliza shule ya mtoto wako kuhusu msaada wanaompa mtoto wako hadi asome katika kiwango cha gredi.

## Je, una maswali?

Tuma barua pepe kwa ThirdGradeGuarantee@education.ohio.gov.

**Januari 2025**